# Uanadini wa Marijani Rajabu na Athari katika Sanaa Yake

*Abel Nyamahanga*
**Idara ya Lugha,Chuo Kikuu cha Kikatoliki Ruaha**
**Email:*Nyamahangaa@yahoo.com***

**Ikisiri**

Makala hii ililenga kuonesha athari ya dini ya msanii katika sanaa yake anayoifanya. Ili kufanikiwa kuliweka bayana wazo hili, ilibidi kuangalia kwa ufupi maisha ya Marijani Rajabu katika dini na sanaa yake. Nyimbo kama vile, *Rufaa ya Kifo, Alinacha, Mama Watoto, Ndoa ya Mateso, Ukewenza, Mwanameka, Ukatili ni Unyama,* na *Nyota Njema* zimetumika ili kubaini maudhui ya kidini yaliyomo. Makala hii ilibaini kuwa sanaa ya Marijani Rajabu iliathiriwa sana na dini yake.

## Utangulizi

Andiko hili limegawanyika katika sehemu nne ambazo ni utangulizi, maelezo kuhusu msanii, maana ya dini na sifa ya sanaa iliyoathiriwa na mtazamo wa kidini, mwelekeo wa kazi yenyewe kuhusu athari ya dini ya mwandishi katika sanaa na hitimisho.

## Maana ya Dini

Dini ni mfumo wa imani ya mtu au jamii kuhusu kile wanachokiamini. Imani ya mtu kuhusu dini huunganisha amali za tamaduni mbalimbali zinazohusisha shughuli za utambikaji. Dini ni kiunzi muhimu katika maisha ya mwanadamu ambacho humtambulisha mtu, jamii ya watu kutokana na kile wanachokiamini (www.amazon.com.Religion.context.). Kwa maelezo hayo, dini ni imani ya mtu juu ya kile anachokiamini katika maisha yake. Kupitia dini, ndipo mtu anaweza kuishi maisha ya aina fulani. Dini nyingi tulizozizoea ni zile zinazomwongoza mtu akaonekana anatenda mema ya mfano katika jamii. Dini inachukuliwa kuwa ni asasi ya maongozi mema. Msanii mkongwe kama vile Shaban Robert kupitia vitabu mbalimbali vya ushairi na riwaya anaonesha kuwa dini ni sifa anayotakiwa mtu kuwa nayo, kwani ndiyo hasa huongoza maisha yake mema. Kazi zake zinatoa mwelekeo kuwa mtu asiye na dini ni kama hayawani, anakosa

utashi wa kibinadamu.

Imani ya dini humwingia mtu kutokana na malezi anayoyapata kutoka kwa wazazi au walezi. Halikadhalika, mtu anaweza akafahamikiwa na dini kutokana na watu wanaomzunguka katika maeneo anayoishi. Kwa mfano, mtoto anayezaliwa atafuata na kuamini kile wanachoamini wazazi wake mpaka katika utu uzima wake atakapoamua kuachana na imani hiyo kwa matakwa yake. Dini hiyo, huweza kuathiri shughuli zake za kila siku.

**Kuhusu Msanii**

Msanii anayeshughulikiwa katika makala hii ni Marijani Rajabu.Alizaliwa mwaka 1954 mkoani Dar es Salaam katika viunga vya Kariakoo.Kwa mujibu wa taarifa ya utafiti uliofanywa na Nyamahanga (2015), anasema kuwa Marijani Rajabu alilelewa katika misingi ya dini ya Kiislamu. Jambo ambalo liliathiri maisha yake na sanaa yake. Katika Maisha yake Marijani Rajabu alikuwa ni mtu wa heshima na mwenye kuheshimu watu wote, wakubwa kwa wadogo.

**Maisha yake Kielimu na Kisanaa**

Marijani Rajabu alisoma shule ya msingi ya Kisarawe hadi mwaka 1970 na baadaye akajiunga na shule yasekondari ya Tambaza mnamo mwaka 1971. Alianza kuimba mwaka 1972 akiwa kidato cha tatu akiwa na umri wa mika 18. Tangu alipoanza kuimba hakuwahi kuupa kisogo muziki hadi kufariki kwake. Alifikia hatua ya kuitwa ***Jabali la Muziki,*** jina ambalo ameendelea kuitwa hata baada ya kifo chake kilichotokea miaka ishirini na mbili iliyopita. Nyamahanga (2015) katika utafiti wake anasema kuwa jina hilo lilitokana na uimbaji wa nyimbo zilizokuwa na maudhui yanayogusa jamii karibu katika kila kipengele cha maisha ya mwanadamu. Nyimbo hizo zilihusu masuala kama vile, kazi, utu wema, malezi kwa watoto, ukombozi wa kifkra na ule wa Makaburu na suala la kifo kama kikwazo cha kwanza cha mipango ya mwanadamu. Vilevle, jina hilo lilitokana na maudhui yake yaliyobebwa na sauti ya aina yake na uteuzi wa lugha katika nyimbo zake. Nyimbo zake zilijaa methali, nahau na misemo mbalimbali ilifanya nyimbo zake zionenekane ni kivutio. Kutokana na hayo, zilitokea kupendwa na watu wengi na nyingine kutumika katika mitihani ya Kidato cha Nne, kama vile wimbo wa

*Mwanameka*. Wimbo huu ulitumika katika mtihani wa taifa wa Kidato cha Nne wa mwaka 1990, jambo ambalo linadhihirisha utaalamu wa Marijani Rajabu katika utungaji wa nyimbo zenye maudhui yanayojitosheleza.

Aidha, Marijani Rajabu alianza kujiunga na*STC Jazz,* bendi ambayoilikuwa chini ya mpiga gitaa maarufu aliyejulikana kwa jina la Raphael Sabuni. Kabla ya hapo, bendi hii ilikuwa inajulikana kama *The Jets.* Mwaka huo huo wa 1972, Marijani alihamia bendi ya *Safari Trippers*. Bendi hii ilikuwa chini ya David Musa ambaye alikuwa mtaalamu wa kupiga gitaa na saksafoni. Waliweza kutoa nyimbo za kuvutia kwa mfululizo bila kupitwa na wakati. Nyimbo kama vile, *Rosa Nenda Shule, Georgina, Mkuki moyoni, Josephina* na mtindo wao wa *sokomoko.* Miezi michache baadaye, Marijani Rajabu na wenziwe walihamia bendi ya Dar *International*. Walipiga nyimbo kama vile, *Zuena* na *Mwanameka* huku mtindo wao wa *supper bomboka* ukitamba. Kwa miezi michache baadaye, Marijani Rajabu alishiriki katika kundi kubwa la wanamuziki 57 waliotengeneza *Tanzania All Stars*, kundi ambalo lilirekodi nyimbo nne ambazo haikuwa rahisi kwa bendi zilizokuwepo kufikia ubora wake kimuziki. Miongoni mwa nyimbo hizo ni *Rambirambi, Fagio la chuma* na *Kifo cha Samora.*

Baada ya safari hiyo ndefu ya kimuziki, Marijani Rajabu aliingia *Mwenge Jazz* kwa muda mfupi, kisha akaimbia *Kurugenzi Jazz* ya Arusha kwa muda wa mwaka mmoja. Baadaye akajaribu kuanzisha kundi lake la *Africulture* na mtindo wa *Mahepe,* lakini kwa ukosefu wa vyombo kundi hili nalo lilikufa. Baadaye Marijani Rajabu akabaki kutembeza CD zake kwenye baiskeli ya miguu mitatu na kuimba kwenye kumbi za starehe. Mpaka anafariki dunia mwaka 1994 alikuwa tayari amekwisha kuandika kwa kalamu ya chuma historia yake kisanaa.

**Sifa ya Sanaa Iliyoathiriwa na Dini**

Kwa mujibu wa Mulokozi (1993), anataja sifa za kazi ya Fasihi ambayo huwa imeathiriwa na imani ya kidini ya mwandishi, sifa hizo ni kama ifuatavyo:

(i) Kazi hizo humtaja Mungu kwa sehemu fulani.

(ii) Huhimiza watu kutenda mema huku zikionesha kwamba mtenda mema atalipwa na Mungu.

(iii) Maudhui yake huonesha kuwa kuna kuishi na kuna kifo pia, na baada ya kifo kuna maisha tena.

(iv) Maudhui yake huhamasisha uvumilivu.

(v) Dhana hii ya uvumilivu inahimizwa sanjari na imani kuwa Mungu hujibu kwa wakati na majira yake.

(vi) Maudhui hugusa hisi za moyoni kwa namna ya pekee.

(vii) Maudhui yake hutawaliwa na mawaidha kwa jamii kuhusu masuala mbalimbali ya namna ya kuishi na jamii.

**Dini na Sanaa ya Marijani Rajabu**

Wapenzi na wachunguzi wa masuala ya muziki wanaamini kuwa athari ya dini yake katika sanaa inaonekana kwenye vipengele vyote viwili yaani, kifani na kimaudhui. Inasemekana kuwa hata sauti yake ilisikika kama vile mtu ambaye alikuwa akiimba Kaswida. Kwa kuanza mjadala kwa kuziangalia sifa hapo juu, tuanze kwa kuangalia sifa moja moja ili kuthibitisha dai la msingi.

**Kutajwa kwa Jina la "Mungu" katika sanaa**

Miongoni mwa nyimbo kadhaa alizoimba Marijani Rajabu zipo nyimbo alizoimba kwa kumtaja mungu. Ingawa Mungu ametajwa kwa namna tatu kama vile Mola, Allah na Mungu lakini, ni yule yule Mungu wa mbinguni. Katika wimbo wa *Rufaa ya Kifo*wenye maudhui ya kwa nini kifo kipo. Kifo ni mpango wa Mungu baada ya mwanadamu kumkosea pale bustanini. Licha ya msanii kulaumu kifo, anajijibu kwa kuonesha kuwa kifo ni mpango wa Maulana. Msanii anasema:

> Kama ingalikuwaa, binadamu anakata *rufaa ya kifooo,ohhh,*
> *inapotokeaaaa,* ***mbele ya Mungu*** *na mimi ningekataa rufaaa,*
> *nirudishiwe wanguuuu niliyempendaaaaa*
> *hapaduniani lakini ninashindwa sijui nifanyeje*

***Lakini Mola yeyeyeeee****,*
*Kazi yake haina makosaaa, (kweli haina makosa)*
*Wala hairekebishwi na binadamu yeyote*
***Yeye ndiye muumbaaaeee****, yeye ndiye muwezaaaa*
*Analotaka amuaaaee, eeeh huwa eee*
***Lakini Mola yeeyee***

Katika wimbo huu msanii anaonesha kuwa Mungu ananguvu na hupanga lolote likafanyika na kwamba pasipo yeye hakuna linalowezekana.

Vilevile, katika wimbo wa *Mama Watoto,* wimbo huo una maudhui ya matendo mema kwa yatima, ikiwemo kuwapa malezi na huduma mbalimbali kwao. Katika kusisitiza mauudhui hayo, msanii anamtaja Mungu katika sehemu ya wimbo kwa kusema:

***Mama watoto muogope Mungu wako****,*
*Kwa huyo mwana asiye na mama,*
***Yeye hakuomba ila ni kazi yake Mungu***
***Kazi ya Mungu haina makosa***
*Uhai, uhai umeumbwa*
*Na kifo vilevile kimeumbwa*,

Dhana inayosisitizwa na msanii ni mwanadamu kumwogopa Mungu katika matendo yanayomwumiza mwingine. Hali yauyatima inatokana na kufiwa na wazazi wote wawili kutokana kifo ambacho kimekuja na mpango wa Mungu. Na hivyo, kwa kuzingatia hilo, msanii anaiasa jamii iwalee yatima kwa kuwapa huduma mbalimbali sawa na watoto wao bila kuwatenga.

Katika nyimbo za *Nyota Njema na Alinacha* Mungu ametajwa mara kadhaa ili kusisitiza maudhui yaliyomo.Maudhui yaliyomo katika nyimbo hizi ni ya kufanana. Maudhui yenyeweyanahusu kutokukata tamaa katika kujitafutia kipato halali. Katika kujitafutia riziki kwa mtu binafsi, kuna watakaodhihaki juhudi za mtu na wengine hawatakubaliana na mafanikio aliyofikia mtu. Msanii katika wimbo wa *Nyota Njema* anasema:

*__Baada ya dhiki Mungu kanikumbuka__, sasa*
*mbona jirani wanisakama buree*
*ooooo jirani oooooooooo jirani oooooooo*
*jirani mbona wanionea bureeee unanisakama*
*bure jirani*.

Katika wimbo wa *Alinacha* msanii anasema:

*Sisi sote tumeumbwa kuhangaika eeeh,*
***Hangaika usikate tamaa Mungu anakuona**,*
*Iko siku utafanikiwa kama wenzio eeh*

Katika wimbo wa *Nyota Njema, msanii* anaonesha kuwa Mungu humbariki yule anayejihangaisha. Kauli ambayo inalandana kabisa na kauli isemayo 'tunda huwa halidondoki mbali na mti wake'. Katika wimbo wa *Alinacha*, msanii anaonesha kuwa kukata tamaa ni dhambi, maneno ambayo yamo katika vitabu vitakatifu.Vitabu hivyo pamoja na masuala mengine vinahimiza umuhimu wa kufanya kazi.

Katika wimbo wa *Ukatili ni Unyama,* una maudhui yanayohusu ukatili wa Makaburu wa Afrika ya Kusini dhidi ya wananchi. Msanii anaonesha kuwa unyama uliofanywa na Makaburu ulikuwa ni unyama uliovuka mipaka ya ukatili kwa binadamu. Akizungumza na kusisitiza maudhui hayo anasema:

*Kuzitoa roho za watu bila sababu ee*
*Hata watoto wadogo wamekosa nini ee?*
***Mtakwenda sema nini mbele ya Mungu ee***
*Makatili tunawapiga lana ee....laana kuubwa..*
*Kila mtenda e atakumbukwa kwa wema.*

Msanii anajiuliza swali kuwa Makaburu hawa kwa ukatili wao watakwenda kusema nini mbela ya mungu. Ukatili unapingwa na Mungu kupitia vitabu vitukufu. Mawazo hayo, yanatuelekeza kwenye imani ya kidini kuwa ukatili wa mtu una mwisho. Na mwisho wa ukatili ni laana ya milele.

Halikadhalika, katika wimbo wa *Sababu ya Mapendo.* Maudhui ya wimbo huu ni kuhusu wazazi kumchagulia mume binti yao ilihali hakuna mapendo kati yao. Katika kuyaeleza na kuyasisitiza maudhui hayo huku akimtaja Mungu msanii anasema kuwa:

*O jama niacheni e.....mwenzenu nimeshapenda jama*
*Walimwengu walikwisha sema kipendacho roho hakina dawa eeee*
*O jama niacheni e.....mwenzenu nimeshapenda jama*
***Asiyejua kupenda Mungu amsaidie yasimkute eee***

Msanii anasisitiza maudhui haya kwa kutaja jina la Mungu kwa lengo la kutaka kuonesha thamani ya mapendo kwa waliopendana. Anaona kuwa kitendo cha kuchaguliwa mpenzi na kumwacha yule aliyempenda na kupendana kwa mapenzi ya kweli ni ukatili. Na ndiyo maana ili kuonesha kuwa anapinga kabisa mpango wa wazazi wake anatamka maneno hayo ya "asiyejua kupenda Mungu amsaidie yasimkute"

Hatimaye, wimbo wa *Namsaka mbaya wangu.* Maudhui ya wimbo huu yanahusu umbeya au uchonganishi. Uchonganishi ni kufanya watu wahitilafiane. Hapa anasema:

*Nikamuelezaa ah mama Maria ...... mama Maria*
*Watu fitina walivyo mambo yao ..... mama Maria*
***Nikaapa kwa jina la Mungu ......... mama Maria***
*Kwamba mumewe sina habari nae hakukubali*

Jina la Mungu hapa limetumika kama kiapo ili kuthibitisha kuwa anayoyasema ni ya kweli. Kwa hiyo, hapa kuna dhana ya ukweli inasisitizwa. Ukweli unasisitizwa katika vitabu vitukufu vya Mungu lakini kuna msemo wa wahenga usemao kuwa ukweli hujitenga na uwongo ni kama mafuta na maji.

Hizo ni baaadhi ya nyimbo ambazo zinataja Mungu. Hata hivyo, ukiachilia mbali kumtaja Mungu lakini bado hata maudhui yake ni elekezi kwa jamii.

**Kuhamasisha jamii Kutenda Mema**

Sifa ya pili ni kuwa na maudhui ya kuhamasisha jamii kutenda mema na kulaani maovu. Kwa mfano, wimbo wa *Mama Watoto* unaomtahadhalisha mama wa kambo aache kumtesa mtoto yatima. Msanii anasema:

*Mama watoto*
*Acha roho mbaya,*
*Nakusihi mama, nakuomba,*
*Au kwa sababu wazazi wake, wametoweka,*
*Si kosa lake mwana hiyo ni kazi ya Molaaa,*
*Huyu ni mtoto sawa na watoto wako,*
*Hebu fanya huruma ,usimtese mwana*
*Oh mama watoto, usimtese mwana,*

Kumtesa mtoto yeyote ni jambo baya lakini kumtesa mtoto yatima linaonekana ni jambo baya zaidi kwa sababu yatima anaonekana anapaswa kuhurumiwa zaidi kuliko wengine kutokana na adha ya kufiwa wazazi. Msanii anaiasa jamii kuwaonea huruma watoto yatima kwa kuwapa mahitaji na si kuwabagua.

Wimbo mwingine unaohimiza watu kutenda mema na kulaani maovu ni wimbo wa *Mwanameka.* Wimbo huu umebebwa na jina la mhusika 'Mwanameka' aliyeparaganyisha ndoa ya Musa. Kitendo hiki cha Mwanameka kimelaaniwa na ulimwengu mzima. Kitendo alichokifanya Mwanameka kinaonekanana ni cha kinyama na cha hujuma kwenye ndoa ya Musa. Unyama huu unadhirika kwa Mwanameka kwa sababu alipogundua kuwa amesababisha madhara kwenye ndoa ya Musa, hakuwa na hamu ya kumwona tena Musa. Jambo hili linauaminisha ulimwengu kuwa lilipangwa. Hapa msanii anasema:

*Kweli Mwanameka umefanya madhambi makubwa*
*Mambo ulomfanyia Musa yanasikitisha*
*Eee Mwanameka mkasa uliofanya ni wa mwaka*
*Ooo bwana Musa hatokushau mpaka kufa*
*Tena amekwisha apa mambo ya upuuzi hataki tena*
*Keshaumwa na nyoka akiona unyasi anashituka*
*Eee Mwanameka hebu punguza matata*

Msanii analiona hili si jambo la wema, ni kinyume cha ubinadamu na mazoea ya ubinadamu. Kupitia wimbo huu, jamii inaaswa kuwa na matendo mema husussani kuwa na heshima kwenye ndoa za watu wengine. Miongozo ya dini inahimiza watu kuzijali ndoa zao na kuheshimu ndoa za watu wengine pia.

Wimbo mwingine unahamasisha kutenda mema ni wimbo wa *Ndoa ya Mateso* wenye maudhui yanayohusu mwanamke aliyetelekekezwa na watoto huku mwanaume akila starehe kwenye majumba ya starehe. Mke na watoto ameachwa bila chakula akibaki kuwa ombaomba ili aweze kuwatunza watoto wake. Wanaume wanakumbushwa kuwa wawe wenye kutenda matendo mema kuanzia kwenye familia zao na baadaye nje ya familia zao. Hapa msanii anasisitiza haya kwa kusema:

*Hapa unapotuona hatuna chochote nyumbani*
*Mume wangu haonekani sijui yuko wapi*
*Anababaishwa na anasa za mjini*
*Bibi kanitupa na watoto hawajali*
*Pesa zake zote zinaishia nje*
*Kwa makuku ya kukaanga*
*Mimi na mkate mkavu*
*Nimechoka mimi na Mwanaume mlevi*
*Heri anipe talaka mimi nirudi kwetu*
*Sikuzaliwa juu ya miti*
*Ninako kwetu(x2) kwa Baba na Mama*

Katika kueleza dhana hii ya kutenda mema, anawatumia wahusika kadhaa ambao wanaonekana kumhurumia sana kwa matendo anayotendewa na mumewe. Katika kutatua mgogoro huo, wanamshauri mwanamke asichukue uamuzi wa kuondoka. Msanii anasema:

*Naona vibaya mmeshazaa watoto*
*Mkitengana mtawapa tabu watoto wenu Mama*
*Mateso, mateso,mateso yamezidi nachokaa*

Upo ushauri wa aina mbili, wapo wanaoshauri kuwa achukue hatua ya kuachana na mumewe ili aupumzishe moyo wake kutokana na maumivu anayoyapata. Pia, kwa upande wa pili wapo wanaoshauri asiondoke nyumbani kwa mumewe kwamba huenda mahangaiko ya mama huyo na watoto yakaongezeka. ili watoto wasihangaike kutokana na kukosa matunzo ya wazazi wote wawili. Kwa pamoja wanamwonea huruma mama huyo.

**Uhai baada ya Kifo**

Nyimbo za Marijani Rajabu zimeonekana kuwa na maudhui yanayoonesha kuwa kuna kifo na kuna maisha baada ya kifo. Imani hii ipo katika vitabu vya dini. Vitabu hivi vinawahimiza waumini watende mema ili kuishi maisha ya furaha peponi. Msanii kaonesha imani hiyo katika nyimbo zake za *Ukatili ni Unyama* na wimbo wa *Mama Watoto.*

Katika wimbo wa *Ukatili ni Unyama,* msanii anasema kuwa *Mtakwendasema nini mbela ya Mungu.* Kauli hii inaonesha kuwa maisha ya mwanadamu hayaishii duniani. Duniani ni mahali ambapo mwanadamu anatakiwa kuishi maisha yanayompendeza Mungu na wanadamu.

Katika wimbo wa *Mama Watoto,* msanii anaonesha imani juu ya kifo na uhai kuwa vyote vimeumbwa na Mungu. Mtunzi wa wimbo anatamka hayo katika kusisitiza kutenda mema kwa ajili ya furaha ya maisha yajayo.

Katika suala la kifo, msanii anaonesha kuwa kama binadamu angeambiwa kuwa kesho ataiaga dunia binadamu asingekutwa amekaa, angekutwa mbali akiwa anakimbia. Lakini kifo hakikimbiwi, kifo ni siri isiyotanzuka. Ndiyo maana, msanii anasema kama kungekuwa na nafasi ya kukata rufaa, basi kila mtu angekata rufaa kwa gharama yoyote na kwa kila namna. Msanii anasema kuwa kama kungekuwa na nafasi ya kukutana na Mungu wangeomba watoto na ndugu zao warudishwe. Kama asemavyo hapa:

> *Kama ingalikuwaaa, binadamu anakata rufaa ya kifooo,ohhh,*
> *inapotokeaaaa, mbele ya Mungu na mimi ningekataa rufaaa,*
> *nirudishiwe wanguuuu niliyempendaaaaa*
> *hapa duniani lakini ninashindwa sijui nifanyeje*

Msanii anakiri wazi kuwa hakuna namna yoyote ya kuweza kukikwepa kifo, vinginevyo Mungu aamue kubadili adhabu hii, jambo ambalo si rahisi. Zaidi ya hayo, binadamu hana namna zaidi ya kukipokea kifo ambacho ni kinyume cha uhai wetu. Msanii haoni sababu ya kumlaumu Mungu, ndiyo maana anasema:

Lakini Mola yeyeyeeee,
Kazi yake haina makosaaa, (kweli haina makosaaa
Wala hairekebishwi na binadamu yeyote.
Yeye ndiye Muumbaaaeee, yeye ndiye Mwezaaaa
Analotaka amuaaaee, eeeh huwa eee.

Hali hii ya kufikia hatua ya kubali na kukipokea kifo inatokana na imani yake kuhusu maisha ya peponi baada ya kifo. Ni rahisi kukipokea kifo kuwa na kije kwa mtu anayeamini kuwa kuna kuishi tena. Kwa mtu asiyeamini hayo, ni vigumu kukipokea kifo. Imani hii tunajengewa kupitia kwenye nyumba za ibada na vitabu vitukufu.

**Kuhimiza Uvumilivu**

Uvumilivu ni suala linalohimizwa kwa namna katika vitabu vitakatifu. Uvumilivu ni kuwa na subira, hali ya kutokukata tamaa katika kusubiri jambo au katika kufanya kazi. Katika vitabu vya dini dhana hii ya uvumilivu ina upana wake mkubwa, kwa mfano, kumwomba Mungu na kubaki kusubiri majibu ya Mungu, kutenda mema bila kukata tamaa kwa ahadi ya maisha ya peponi. Huu ni uvumilivu. Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa uvumilivu anaouzungumzia msanii katika nyimbo zake umeota mizizi kutoka kwenye vitabu vitakatifu vya Mungu. Aidha dhana hii ya uvumilivu inaonekana kupitia nyimbo za *Ndoa ya Mateso,Ukewenza na Alinacha*.

Maudhui ya wimbo wa *Alinacha* yanasisitiza umuhimu wa kazi, na kwamba watu hawatakiwi kujichagulia njia zisizo njema au za mkato za kujitafutia kipato Zipo njia ambazo ni sahihi katika kumletea mtu kipato lakini uvumilivu unahitajika. Akihamasisha uvumilivu katika kazi msanii anasema:

*Sisi sote tumeumbwa kuhangaika eeeh,*
*Hangaika usikate tamaa Mungu anakuona,*
*Iko siku utafanikiwa kama wenzio eeh*
*Fanya kazi.*

Vievile katika wimbo wa *Ndoa ya Mateso*, unasisitiza uvumilivu kwa binadamu. Msanii anasema:

*Ni mateso, mateso mateso yamezidi nachoka*
*Pole Mama kwa tabu unazopata*
*Lakini kwanza usichukue hatua hiyo mama*

Hali ya kuteswa na ndoa yake inaonekana ilianza tangu kitambo. Uthibitisho wa maelezo ya msanii hapo juu yanaonesha namna mwanamke alivyoishi kwa kuvumilia ndoa hiyo licha ya kuwa na mateso makali. Pamoja na mwanamke huyu kuwa ameamua kuachana na mateso, uamuzi wake unapingana na mawazo ya mjumbe anayemwambia kuwa asichukue uamuzi wa kuondoka. Wazo hilo nalo bado linajenga dhana ya uvumilivu.

**Maudhui yake Huwa na mguso mkubwa kwa wasikilizaji**

Kazi za ya Fasihi ambayo maudhui yake yana mizizi ya kidini huwa na mguso wa moyo kwa namna ya pekee. Hii inaweza ikawa ni kutokana na visa ambavyo husukwa kiasi cha wasikilizaji kuwaonea huruma wahusika. Vile vile, visa hivi hubeba ujumbe mzito kwa jamii. Nyimbo za Marijani Rajabu zina visa ambavyo vinasimuliwa katika hali ambayo huwafanya wasikilizaji waambae na msimuliaji. Nyimbo za Marijani Rajabu pia, maudhui yake yana mguso ambao msikilizaji anaupata kutokana na jumbe zilizomo. Kwa mfano, wimbo wa *Ukewenza, Ndoa ya Mateso,Mwanameka, Ukatili ni Unyama, Mama Watoto* nk. Ni nyimbo ambazo ukizisikiliza zina msisitizo wa maudhui ya maadili, maonyo na miongozo mbalimbali ya maisha ya kila siku ya mtu. Mgoso huo kwa wasikilizaji unataokana na visa vilivyomo katika nyimbo hizo kusawiri uhalisi. Msikilizaji anaguswa kiasi cha kuona kuwa visa vinavyowahusu mama, dada, kaka na majirani zetu katika mazingira haya na yale.

**Maudhui ya Nyimbo huwa ni Mithili ya Mawaidha**

Maudhui ya nyimbo za Marijani Rajabu zilizo nyingi ni za kimawaidha. Mawaidha ni mafundisho kuhusu masuala mbalimbali. Mawaidha haya yanaweza kuhusu umuhimu wa kuheshimu wazazi, umuhimu wa dini kwa jamii, kuheshimu ndoa, maadili, kazi nk. Ni maudhui yenye mwelekeo wa mahubiri ya nyumba za ibada. Msanii ameyazungumzia masuala muhimu yanayoihusu jamii kwa mapana na kwa mkazo, huku akionesha matokeo ya kuyashika mafundisho hayo na athari za

kutokuyashika. Msanii anaonesha kuwa matokeo ya kushindwa kuzingatia mafundisho mema ni hukumu ya duniani na ya Mwenyezi Mungu huko ahela. Haya yameonekana katika nyimbo za *Ukatili ni Unyama*, Mama *Watoto*n.k. Mafundisho anayoyazungumzia msanii na kuyasisitiza yanaonekana kuwa na msingi katika vitabu vya imani ya dini.

**Nafasi ya Dini katika Jamii**

Dini iliyochorwa na msanii katika nyimbo zake ni ile iletayouhusiano kati ya mwanadamu na nguvu za asili zilizo mbinguni ambazo ndizo chanzo cha uhai wake. Msanii anaamini kuwa katika uumbaji wa dunia na vitu vingine, Mungu aliumba uhai na kifo kama ilivyoandikwa katika vitabu vitakatifu.

Msanii anaamini kuwa kama binadamu wote tutakubali kuishika dini, amani itakuwa kila kona ya dunia. Kwa sababu kila mtu ataogopa kutenda maovu kwa kuogopa kukosana na Muumba wake. Mtu anayemwogopa Mungu hataiba, hatavunja ndoa ya mwingine, hataua namatokeo yake itakuwa ni amani tele. Kwa hiyo, msanii anaiasa jamii ishike dini ili, si tu waishi vema hapa duniani, bali kupokelewa na Mungu peponi. Kwa kufuatilia tu mistari inayotaja Mungu katika nyimbo zake kama vile, *utasema nini kwa Mungu, mwogope Mungu, kazi ya Mola haina makosa, Malipo kwa Mungu, Mungu anaona kuhangaika kwako*, *kifo na uhai vimeumbwa,* utagundua kuwa msanii anatoa mwongozo kwa jamii. Kwa hiyo, Marijani Rajabu anaona kuwa dini ni kiunganishi cha mtu na mtu, na vile vile ni kiunganishi cha mwanadamu na Mwumba wake. Na kwamba matendo mabaya ndiyo yanayochafua dunia na kumtenga binadamu na Mungu wake. Sanaaa yake inaonesha kuwa mtu asiye na dini ni kama hayawani, ni mtu asiyeogopa chochote, na ni mtu anayeweza kuwatendea wenziwe mabaya na hata mauaji. Katika wimbo wa "Ukatili ni Unyama" anawalaumu Makaburu kwa mauaji ya watu na watoto wa Afrika Kusini, kwa kuwauliza kuwa hawamwogopi hata Mungu. Maana kama wangekuwa na hofu ya Mungu mioyoni mwao wasingewaua wala kuwatesa watu.

Marijani Rajabu kupitia sanaa yake anaonekana kuamini kuwa maisha ni majaliwa ya Mwenyezi Mungu kama ilivyo kwa kifo. Kwa hiyo, kukosa au kupata ni kudra za Mwenyenzi Mungu. Imani

yake inaonesha kuwa wanaojaliwa kupata ni wale wanao mcha *Allah,* na wale wa kukosa pia, hutokana na kutomtiii Muumba wao.

**Hitimisho**

Makala hii ilikuwa inaangalia imani ya msanii katika dini na athari yake katika kazi ya sanaa. Imeonekana kuwa katika nyimbo nyingi za Marijani Rajabu zimeonekana kuathiriwa na imani yake. Marijani Rajabu katika nyimbo nyingi anaonesha kuwa Mungu anachukia uovu wa mwanadamu. Uovu ambaohata vitabu vitukufu hususani,Quranikitabuambacho yeye alikiamini kinakataza maovu. Baaadhi ya surati ambazo zinashikamna na maudhui ya nyimbo zake nisurati ya 3:36 inakataza roho mbaya ya maovu na 3:145 inasema kuwa zawadi ya mtenda mema ipo hapa duniani na mbinguni pia. Halikadhalika, adhabu ya mtu mwovu ni duniani na mbinguni. Kwa hiyo, Uislamu wa Marijani Rajabu umedhihirika kwenye sanaa yake. Hivyo, niseme kuwa si rahisi sanaa ikawa huru dhidi ya imani ya dini ya mtunzi. Hii ina maana kuwa kile anachokiamini mtu katika dini yake ndicho ambacho mara nyingi hukitamka. Kwa Marijani Rajabu ni kuwa imani yake ya dini ilimwathiri kwa kiasi kikubwa.

**Marejeleo**

Mulokozi, M. M. (1993). Misingi ya Uhakiki wa Fasihi, English Press Ltd, Nairobi- Kenya.

Nyamahanga, A. M. (2015). Athari za Miktadha ya Kijamii katika Muziki wa Dansi Tanzania: Mifano kutoka Nyimbo za Marijani Rajabu. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu ya Chuo Kikuu cha Dodoma.